BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 02 Oktoba, 2024
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

182. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

(a) Kuna tafiti na tathmini ngapi na zipi zimefanyika katika suala zima la kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi mpaka sasa.

(b) Ni tafiti zipi kati ya hizo zimeweza kuleta au kusaidia kupatikana ufumbuzi unaohitajika.

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

21. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Serikali inafanya juhudi kubwa katika kuhamasisha ulipwaji wa kodi, hata hivyo, zipo baadhi ya kodi husamehewa kwa mujibu wa sheria.

Je, ni zipi faida na tija za kodi zinazosamehewa kwa taifa letu.

Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

140. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni kwa kiasi gani Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) inapambana na viashiria pamoja na vitendo vya rushwa katika muktadha mzima wa Sekta ya Uwekezaji.

240. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Katika hatua za kuimarisha usalama na afya kazini, Serikali ilianzisha Idara ya Usalama na Afya Kazini ili kuhakikisha mazingira ya kazi yanakuwa salama kwa wafanyakazi. Hata hivyo, Idara hii inakabiliwa na changamoto nyingi zinazoathiri utekelezaji na ufuatiliaji wa sera na sheria zinazohusiana na usalama kazini kwenye sekta za umma na sekta binafsi.

(a) Je, Serikali inatambua tatizo hili na ni mipango gani inafanyika ili kuiwezesha Idara katika kuboresha usimamizi na utekelezaji wa sheria za usalama na afya kazini.

(b) Je, ni kesi ngapi za ukiukwaji wa Sheria ya Usalama Kazini ya mwaka 2005 zimewahi kuripotiwa, na hatua zipi za kisheria huchukuliwa kwa waajiri.

(c) Je, Idara ya Usalama na Afya Kazini ina mpango gani wa kutoa mafunzo na elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili kuongeza uelewa na utekelezaji wa viwango vya usalama na afya kazini.

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

169. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali imeruhusu uwepo wa redio, televisheni, magazeti na hata mitandao binafsi ya kijamii kwa lengo la kukuza wigo mpana wa uhuru na demokrasia ya vyombo vya habari nchini.

(a) Je, hali hii imeifanya Zanzibar kuwa na redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii mingapi inayomilikiwa na watu binafsi.

(b) Je, Zanzibar inapata asilimia ngapi ya kodi kutokana na vyombo hivi.

(c) Kwa kiasi gani Serikali imeweza kuvisimamia vyema vyombo hivyo katika kulinda maadili, mila, silka, na utamaduni wetu.

178. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Licha ya kufanya vizuri katika tasnia ya habari kwa 'Azam Television' kumekuwa na malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi juu ya kupanda kwa gharama mara kwa mara kwa vifurushi Azam.

Ni ipi kauli ya Serikali katika udhibiti na usimamizi wa huduma zinazotolewa na mashirika binafsi juu ya kupanda kwa gharama hizi za vifurushi.

<u>Wizara ya Afya:</u>

150. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

(a) Kuna tofauti ipi kati ya usajili wa maduka ya madawa maarufu kama 'pharmacy' na maduka ya madawa ya asili.

(b) Je, kuna ulazima wowote ule wa kwamba madawa ya asili kupatiwa nembo ya ZFDA.

(c) Ni utaratibu gani unaotumika katika utengenezaji wa dawa za asili mpaka kuweza kuruhusika kutumika na kuuzwa.

279. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na nia njema ya Serikali ya kutoa vyakula kwa wagonjwa wanaolazwa katika Hospitali za Serikali, kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi na wagonjwa kuhusu huduma hii. Malalamiko haya yanaonesha kwamba katika baadhi ya hospitali, hasa katika kisiwa cha Pemba, huduma hii bado haijaratibiwa vizuri.

(a) Je, Serikali inashughulikia vipi malalamiko yanayohusu utaratibu mbovu wa utoaji wa vyakula kwa wagonjwa katika hospitali za kisiwa cha Pemba.

(b) Je, ni upi utaratibu rasmi wa Serikali katika kutoa vyakula kwa wagonjwa katika hospitali za Serikali, na vipi utaratibu huu unatekelezwa ili kuhakikisha ubora wa huduma unazingatiwa.

(c) Je, Serikali hutenga kiasi gani cha fedha kwa mwaka kwa ajili ya huduma ya vyakula katika hospitali za Wilaya, na vipi fedha hizi zinagawanywa na kusimamiwa kwa kuhakikisha huduma bora kwa wagonjwa inapatikana.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

259. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kumekuwa na malalamiko kwa wananchi juu ya kupanda kwa bei ya umeme wanaponunua kwa kutumia mfumo wa kidigitali tofauti na pale awali ambapo walikuwa wakinunua vibandani. Jambo hili limeleta usumbufu mkubwa kwa watumiaji hawa wa umeme hapa Zanzibar.

(a) Ni ipi kauli ya Serikali juu ya kupanda kwa bei ya umeme hapa Zanzibar.

(b) Je, kwa sasa gharama za umeme ‘unit’ moja ni kiasi gani ukilinganisha na bei ya awali na mapato ya kiasi gani Serikali hupata kwa ongezeko hilo.

(c) Ni mashirika yepi Serikali imeingia nayo mkataba kwa ajili ya kuuza umeme kwa mfumo wa kidigitali.

263. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na juhudi kubwa za Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) za kuwaunganishia umeme wananchi, tatizo la kuchakaa na kuharibika kwa nguzo za umeme mara kwa mara linaendelea kuwa changamoto kubwa katika utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

(a) Je, kwa tathmini ni nguzo ngapi za miti hutumika kwa mwaka na kiasi gani cha fedha zinazotumika kununulia nguzo hizo.

(b) Kwa kuwa hivi sasa ni muda muafaka wa kutumia nguzo za zege badala ya nguzo za miti, ni lini ZECO itaanza kuzitumia nguzo hizo ili kutunza mazingira na faida nyengine zilizopo.

(c) Je, Shirika limefanya tathmini ya gharama na faida za kutumia nguzo za zege ikilinganishwa na nguzo za miti na matokeo ya tathmini hiyo yameonesha nini.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

109. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Baadhi ya kozi zinazofundishwa katika vyuo vikuu vyetu hapa Zanzibar zinaonekana wazi kwamba zinampa mhitimu changamoto ya kuweza kuajirika kwa muktadha wa mahitaji ya soko la ajira katika sekta binafsi na Serikalini.

Je, Wizara yako imefanya tathmini gani inayothibitisha uwepo wa changamoto hii.

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Maboresho ya mtaala mpya wa umahiri hayawezi kamwe kuyapa kisogo mafunzo ya taaluma ya ubunifu.

(a) Ni utaratibu gani unaotumiwa na Wizara yako katika kuwapatia walimu mafunzo haya ya ubunifu ili kwenda sambamba na lengo zima la utekelezaji kwa vitendo la mtaala mpya wa kupima umahiri.

(b) Ni walimu wangapi mpaka sasa wameshapatiwa mafunzo haya ya ubunifu na ni katika fani zipi.

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:

68. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kutokana na athari za UVIKO katika Sekta ya Utalii, Serikali ilifanya maamuzi ya kufungua masoko mapya hususani katika nchi za Ureno, Poland, na Ujerumani.

Je, tathmini iko vipi juu ya matokeo chanya ya mkakati huo.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

118. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Tathimini ya matumizi ya mbolea za kemikali ipo vipi katika uzalishaji wa mazao mbali mbali ya kilimo.

(b) Ni upi utaratibu mzuri wa kutumia mbolea hizi za kemikali ili kuweza kupunguza madhara kwa mlaji.

163. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini iko vipi juu ya utaratibu wa kuwatia ng'ombe shemere kwa muktadha wa haki stahiki za wanyama wa kufugwa.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

160. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Hifadhi za bahari ndio msingi wa uimara wa Uchumi wa Buluu.

(a) Je, tuna hifadhi ngapi hapa Zanzibar kupitia bahari zetu.

(b) Kwa kiasi gani hifadhi hizi zinachangia pato la taifa na kuwa kichocheo kikubwa cha utalii wetu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

100. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ifikapo mwaka 2050 sayansi na teknolojia itakuwa ndio dira kubwa itakayoongoza uchumi wa dunia, bila ya kusahau kuwa Tanzania nayo ni sehemu ya dunia hiyo.

Kwa kiasi gani Wizara imeanza mikakati ya kuwafunda vijana kuelekea kwenye safari ya mabadiliko hayo.

Zanzibar,
02 Oktoba, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA